Tahakiki ya Majukumu ya Mwanamke Katika Tendi Teule za Kiswahili: Utendi wa Fumo Liyongo na Mikidadi na Mayasa

Jackson Ndung'u
Ndururumo Secondary School, Nyahururu, Kenya

Abstract
Swahili epics have been around for a very long time particularly in East African Coast and have been very fundamental in development of Kiswahili language. Swahili epics are among the first works to be preserved in writing. In many literary works, women roles have been portrayed negatively despite the fact that they have played very important roles in development of various aspects in literature. This research investigated the roles of women in Swahili African epics. In many African epics, especially those in Swahili, there are very many women characters that play very important roles, but their efforts are not recognized as compared to men protagonists. The research dealt with two Swahili epics which are; ***Utendi wa Fumo Liyongo and Utendi wa Mikidadi na Mayasa.*** *The objective of the research was to analyse roles of women in the selected Swahili epics. The research was guided by The Archetypal Heroic Theory as espoused by Joseph Campbell. The theory assisted the researcher to collect and analyse data in response to the stated objective. It also helped in setting the scope of the study. The research entailed reading texts and other research concerning the topic to get data. The research was largely conducted in the library. Data was analyzed using qualitative methods in view of the research objective and theoretical premises. The research found that despite the fact that women play a very important role in development of various aspects in Swahili, epics are very critical in the achievement and success of male protagonist and their roles are not recognized and appreciated as compared to male protagonists. The researcher recommends that future researches may investigate the effects issues like religion on women roles in epics.*

Keywords: Epics, heroes, heroes' quest and aspirations, realism, Women roles.

Ikisiri
Tendi za Kiswahili zimekuwepo katika maeneo ya Afrika Mashariki kwa muda mrefu sana na zina umuhimu wa kipekee katika kukuza na kuendeleza maswala mbalimbali ya kijamii, kimazingira na hata katika lugha. Utendi kulingana na Wagiriki wa kale hutokana na neno, hadithi, shairi na ushairi mrefu wa kisimulizi. Kikawaida unaohusu mada kuu inayoshughulikia matukio na shughuli za kishujaa yanayoashiria itikadi au taifa. Katika fasihi kwa ujumla, wanawake wamekuwa wakitekeleza majukumu muhimu sana licha ya kuwa wamesawiriwa kwa mtazamo hasi mno na mchango wao haujashughulikiwa kikamilifu. Utafiti huu ulihusu kutathmini mchango wa mwanamke katika tendi teule za Kiswahili. Katika tendi, hususan zile za Kiswahili, kuna wahusika wengi sana wa kike ambao wanatekeleza majukumu mengi mno na ya kimsingi lakini majukumu yao hayajatambuliwa ila wanaosifiwa ni mashujaa wa kiume tu. Madhumuni makuu ya utafiti huu yalikuwa ni kuhakiki majukumu ya wahusika wa kike katika tendi za Kiswahili. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliyoasisiwa na Joseph Campbell na kuhakikiwa na Timothy Lynns. Utafiti huu ulifuata muundo wa uchanganuzi wa matini ambapo maelezo yetu yaliangazia mchango wa mwanamke katika tendi. Makala ya kimsingi ya utafiti huu yalikuwa kusoma tendi tuele za Kiswahili ilhali makala ya sekondari yalitokana na usomaji wa vitabu na makala yaliyohusu mada. Mtafiti aliteua kimaksudi Utendi wa Fumo Liyongo na Utendi wa Mikidadi na Mayasa kwani tendi hizi ni mojawapo ya tendi maarufu katika Afrika Mashiriki na zingempa mtafiti data aliyonuia

kuitafuta. Pahali pa utafiti palikuwa ni katika maktaba za kitaifa na vyuo mbalimbali nchini Kenya. Ilibainika kuwa licha ya kuwa kwa muda mrefu wanawake katika fasihi wanasawiriwa kwa mtazamo finyu, wanatekeleza jukumu la kipekee katika tendi za Kiswahili. Inanuiwa kuwa utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa mno katika jamii ya usomi hususan kuhusu suala la wanawake katika tendi.

Maneno muhimu: Jaala, majukumu ya mwanamke, shujaa, tendi, uhalisia.

Utangulizi

Tendi za Kiswahili zimekuwepo kwa muda mrefu sana hususan katika maeneo ya Kiafrika kwani ndizo baadhi ya kazi za kwanza kabisa katika Kiswahili kuwekwa katika maandishi. Dhana ya tendi imetazamwa kwa mitazamo tofauti ambayo wakati mwingine hutofautiana. Ufasili wa tendi umekuwa ukielezwa kwa kuangalia sifa. Wataalamu mbalimbali wamejaribu kufasili dhana ya tendi kama ifuatavyo.

Casco (2007) anaeleza kuwa utendi umetokana na kitenzi ‘tenda’ ambacho kinamaanisha kufanya tendo. Anabainisha kuwa utendi huwa na mistari minne yenye silabi nane kwa kila kipande. Mistari huwa na muungano wa matukio. Unaweza kuhusu falsafa au masuala ya kidini, unaweza kutoa simulio la ukweli au la kubuni na huwa unaeleza kuwa kuna ugumu katika kutafuta kisawe mwafaka cha utendi katika lugha mbalimbali.

Wamitila (2003) amejadili utendi kama shairi refu la kisimulizi, linalozungumzia kwa mapana na mtindo wa hali ya juu matendo ya mashujaa au shujaa mmoja. Anasema kuwa utendi huwa na sifa nyingi na huweza kuleta pamoja hadithi ya shujaa, maghani, visasili historia pamoja na ndoto za taifa fulani. Mulokozi (1996) anaeleza utendi ni ushairi wa matendo. Ni utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Matukio hayo yanaweza kuwa ya kihistoria na visakale.

Kutokana na ufafanuzi huu kuhusu utendi, ni dhahiri kuwa utendi ni mojawapo wa utanzu katika fasihi wenye umuhimu wa kipekee katika wanajamii wa taifa lolote lile. Hii ni kwa sababu tendi hushughulikia masuala halisi yanatendedeka na kuenziwa katika jamii na huchukuliwa kwa udhati wa hali ya juu. Kwa hivyo, ni nyema kuchambua masuala ya kijamii kama yanajitokeza katika tendi hizi ili kutathmini ufaafu wao katika jamii husika.

Suala la uhakiki wa nafasi ya mwanamke katika fasihi kwa muda mrefu limezua utata mwingi. Utata huu unatokana na rai kuwa wanawake wamepatiwa nafasi ya chini mno na majukumu yao yanaonekana kutotiliwa maanani sana katika uchambuzi wa kazi ya fasihi, licha ya wao kuwa na jukumu muhimu na la kipekee katika kumkuza shujaa na kuendeleza vipengele mbalimbali katika tendi kama inavyodokezwa na Ndung’u (2016). Pia, Mohamed (2016) alibainisha kuwa wanawake wa visiwani wanatazamwa kwa mtazamo finyu mno na juhudi zao hazijatambuliwa kama inavyodhihrika miongoni wa wahusika wa kiume katika tendi husika kutokana na mila kandamizi zinowakandamiza wanawake.

Kruger (1998) anadokeza kuwa waandishi wengi katika fasihi hawatumii wahusika wanawake kama wahusika wakuu, lakini mara nyingi huwatumia kama wahusika wajenzi hivyo wanabagua kuwasawiri. Mulila (2007) anachanganua usawiri chanya wa wahusika wanawake katika tamthilia ya *Zilizala* na *Chamchela.* Anaangalia jinsi wahusika wanawake na wahusika wanaume wanavyochangia katika kueneza picha chanya ya wanawake. Amechunguza pia itikadi hasi kumhusu mwanamke. Kwa muhtasari tu, watafiti fulani wamedhihirisha kuwa kwa kweli, mwanamke anapewa majukumu hasi na juhudi zake katika fasihi hazijatambuliwa na ikiwa zimetambuliwa, ni katika mawanda finyu mno ikilinganishwa na wanaume.

Wanawake katika tendi wana nafasi muhimu sana kwani kwa wakati mwingi, wao wanakuwa ndio nguzo kuu katika kukuza na kuendeleza sifa tabia za wahusika mashujaa na pia kukuza vipengele mbalimbali vya kifani katika tendi kama vile kukuza ploti, kuendeleza

mbinu mbalimbali za lugha na kuibua motifu fulani. Kwa hivyo utafiti huu ulishughulikia jinsi mwanamke anatekeleza majukumu makubwa na ya kipekee katika kukuza shujaa na kuendeleza tendi za Kiswahili licha ya kudhalilishwa katika jamii.

Utafiti huu ulishughulikia tendi mbili za Kiswahili ambazo ni *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utendi wa Fumo Liyongo*. Sababu ya kuchagua tendi hizi mbili ni kuwa, licha ya kuwepo kwa tendi nyingi za Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki, tendi hizi zinasawiri dhana ya ushujaa, wahusika walio na sifa za kishujaa na pia zinashughulikia nafasi ya mwanamke kwa shujaa na katika tendi kwa ujumla.

Msingi wa Nadharia

Makala haya yaliongozwa na nadharia ya Ruwaza ya Shujaa iliasiwa na Campbell (1949) na kuhakikiwa na wanafalsafa wengine wa fasihi na soshiolojia kama vile Rank (1999) na Lynns (2009). Campbell alidokeza kuwa ili shujaa katika tendi aweze kuafikia jaala yake, lazima apitie hatua mbalimbali zitakazomwezesha kuafikia azma ile. Campbell (1949) alidokeza misingi mitatu katika nadharia hii. Kwanza, ni kuondoka kwa shujaa. Katika kitengo hiki, Campbell anadokeza kuwa ni sharti shujaa aondoke katika taifa lake na aiache jamii yake. Alidokeza kuwa kuondoka huku huwa na visababishi kadha wa kadha. Kwanza kabisa, shujaa hupata mwito. Pili, shujaa hukataa mwito ule na kuamua kushauriana na wanajamii wake au miungu na la mwisho, huamua kuondoka baada ya kushauriana na wanajamii wake au miungu.

Msingi wa pili ni kufundwa na kushindwa kwa shujaa. Katika kitengo hiki, shujaa hupatana na mambo kadha wa kadha. Shujaa hujitenga na kuishi peke yake pale ambapo baadaye hukumbana na adui ambaye hupigana naye vita vikali. Shujaa hujitenga tena na baadaye kukabiliana na adui wake tena katika vita vikali mno.

Mhimili wa tatu ni kurejea na kurudi nyumbani kwa shujaa. Baada ya kushidwa na maadui pamoja na mahasidi wake, shujaa huamua kurejea nyumbani ili aweze kuungana na wanajamii wake. Anaporudi nyumbani, shujaa hukumbana na adui mwingine na vita vingine vikali huzuka pale ambapo wakati mwingi huibuka mshindi. Shujaa hurejea nyumbani akiwa amebadilika. Rank alichangia nadharia hii kwa kudai kuwa mhusika mkuu katika tendi huwa kwa wakati mwingi amezaliwa kutoka kwa tabaka la juu. Anadai kuwa kuzaliwa kwa mhusika huyu hukumbwa na matatizo fulani na huwa kwa njia za kimiujiza na anguko lake husababishwa na usaliti wa mtu wa tabaka la chini au mwanajamii wa karibu. Lynns (2009) alihakiki maoni ya Campbell na kudai kuwa licha ya Campbell kudai kuwa wahusika wakuu katika tendi ni wanaume tu, kuna idhibati kuwa kuna kazi zingine za kifasihi ambapo wahusika wakuu ni wanawake. Alidokeza pia kuwa kwa ajili ya kuwepo kwa tamaduni mbalimbali za kijamii na kutengana kwa misingi ya kijiografia, kuna uwezekano wa tendi mbalimbali kukosa kuhusisha vipengele vyote vya Campbell. Kwa mujibu wa makala haya, mihimili ya kuondoka kwa shujaa, kufundwa kwa shujaa na shujaa kurejea nyumbani ilimsaidia mtafiti pakubwa kwani ni kupitia kwa vipengele hivi ndipo mhusika wa kike hukumbana na kutagusana na shujaa katika tendi na kutekeleza majukumu ya kipekee kwake. Pia, mawazo ya Lynns yanathibithisha kuwa kwa kweli, mwanamke ana nafasi muhimu katika tendi.

Majukumu ya Mwanamke kwa Shujaa katika Tendi Teule za Kiswahili

Kwa mintaarafu ya madhumuni katika utafiti huu, majukumu ya wahusika wanawake katika tendi yalishughulikiwa. Senkoro (1987) ameonyesha kuwa katika fasihi ya mfumo wa kibepari, wanawake daima wamesawiriwa kama pambo la kutamaniwa na wanaume. Anaendelea kudai kuwa licha ya mtazamo huu hasi kuwahusu wanawake katika kazi ya fasihi, wao huwa na jukumu muhimu sana katika kuendeleza maudhui, dhamira na wahusika wengine katika fasihi, wao pia kwa wakati mwingine huweza kuwa ndio washirikishi wa

wahusika wakuu na huwa na jukumu la kipekee katika kuendeleza na kuufanikisha utendi wenyewe. Maoni haya yanaonyesha kuwa wahusika wanawake huwa na nafasi muhimu sana katika fasihi yoyote ile.

Gu'nberg (1987) alidokeza kuwa wanawake katika tendi hizi walikuwa na nafasi hasi mno wakilinganishwa na wanaume. Lakini anaendelea kudai kuwa licha ya hayo, imebainika kuwa ilikuwa ni vigumu kwa wanaume waliokuwa wahusika wakuu na mashujaa katika tendi hizi kuishi peke yao. Hii ni kwa sababu wanawake walikuwa na nafasi muhimu sana katika tendi hizi. Ili kuafikia jaala zao, iliwapasa mashujaa hawa kuwahusisha wanawake ambao wana jukumu la kimsingi sana katika maisha yao. Kwa mujibu wa utafiti huu imedokezwa kuwa kwa kweli, wanawake hawakudhaminiwa katika jamii ya tendi hizi mbili licha ya kuwa wao wanatekeleza majukumu ya kipekee mno kwa shujaa. Pengine mtazamo hasi wanaopewa wanawake kutokana na mitazamo ya kitamaduni na asasi za jamii ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikimkadamiza mwanamke na kumdhamini mwanamme.

Majukumu ya Mwanamke katika Utendi wa Fumo Liyongo

Katika utendi wa Fumo Liyongo, wanawake wanasawiriwa kuwa ni wahusika wenye kuwajibika hususan kwa mhusika wakuu. Katika utendi huu, mamake Liyongo anawajibika vilivyo hususan katika kumlea mwanawe ijapokuwa anapewa nafasi finyu katika utendi wenyewe. Alipokuwa gerezani, alihakikisha kupitia Sada kuwa mwanawe (Fumo Liyongo) hakuwa na njaa kwani kila uchao alitayarisha chakula. Haya yanajitokeza katika ubeti wa 101.

Ubeti 101

Mamake kwa hakiki
Chakula chema kipika
Asikari humpoka
Chakula wakaila.

Anapoelezwa na Sada kuwa Fumo Liyongo kupitia ushairi alidai awekewe tupa katika mkate wa wishwa, mamake Liyongo anatimiza yale. Sada pia kama mwanamke katika utendi huu anawajibika kwani anahakikisha kuwa kila wakati anapopatiwa chakula na mamake Liyongo, anakiwasilisha hadi kwa Liyongo gerezani. Hili ni jukumu kubwa mno lililotekelezwa na wanawake hawa wawili kwani kama haingetendeka vile, Fumo Liyongo angeishia kufia gerezani.

Wanawake katika utendi wa Fumo Liyongo pia wanasawiriwa kuwa wakombozi. Mamake Fumo Liyongo anatekeleza jukumu la ukombozi hususan wakati anaweka tupa kwenye mkate wa wishwa kama alivyodai Liyongo. La msingi ni kuwa, ni kupitia tendo hili ndiposa Fumo Liyongo aliweza kujikomboa kutoka gerezani. Sada pia kama mwanamke anaonekana kuendeleza ukombozi kwa mhusika mkuu ambaye ni Fumo Liyongo. Kwanza kabisa, Sada anapopatiwa ujumbe na Fumo Liyongo kupitia ushairi aweze kumpasha mamake amtilie tupa katika mkate wa wishwa, anatekeleza yale. Pili, Sada kama mhusika wa kike anachukua jukumu lake yeye mwenyewe na kuupeleka tupa ikiwa ndani ya mkate wa wishwa hadi gerezani alipokuwa Fumo Liyongo ambayo baadaye inamsaidia kujikomboa. Haya yanadhihirika katika beti za 104 na 106.

Ubeti 104

Kamba Sada nakutuma
Enda kamwambie mama
Afanye mkate mwema
Kati tupa ativa

Ubeti 106

Mkate huu sikiya
Pishi mbili hutimiya
Kati tupa akativa
Liyongo kampekeya

Mifano hii inayoonyesha wazi kuwa wanawake wana jukumu la kipekee mno kwa shujaa kwani ni kupitia kwao ndiposa Fumo Liyongo aliweza kujikomboa kutoka gerezani. Katika utendi wa Fumo Liyongo, wake wana jukumu na umuhimu wa kipekee hususan kwa wahusika wakuu. Wanawake kwa mujibu wa utendi huu wana jukumu la kuolewa na wanaume na kuzaa watoto nao. Fumo Liyongo alipofika katika makazi ya Wagalla na kuonyesha umahiri wake, wanajamii wa huko walitaka sana kumtafutia mwanamke mrembo kutoka kijiji kile ili awazalie mtoto wa kiume. Linalojitokeza ni kuwa katika jamii hii, mhusika aliyekuwa shujaa alikuwa amependwa sana na wanajamii na ndiposa kizazi chake kiendelee, ilibidi ampate mwanamke na wazae watoto kama inavyodhihirika katika ubeti wa 41.

Ubeti 41

Twaitaka mbegu yake
Nasi kwetu tuipeke
Kwa furaha tumuweke
Apate kutuzaliya.

Linalodhihirika ni kuwa mwanamke ana umuhimu wa kipekee katika kuendeleza kizazi cha shujaa. Katika ubeti wa 46, inadokezwa kuwa Fumo Liyongo aliweza kumpata mwanamke ambaye alichukua mimba na kumzalia mwanamume wa kipekee aliyekuwa na sifa za kishujaa kama zake. Mamake Liyongo pia alikuwa na jukumu kubwa mno la kumzaa Fumo Liyongo ambaye baadaye anakuwa mhusika maarufu sana katika utendi mzima. La msingi ni kuwa, kama Fumo Liyongo hangezaliwa na mamake, kuna uwezekano kuwa hatungekuwa na utendi wa Fumo Liyongo.

Wanawake pia katika utendi huu wana jukumu la kuwa nguzo kuu katika familia zao. Kwanza kabisa, mamake Liyongo ana jukumu kubwa sana katika jamii yake kwani yeye ndiye anayetekeleza jukumu la kumlea na kumtunza Liyongo hadi akawa mtu mzima. Kwa mfano, mama huyu anampikia Fumo Liyongo chakula kitamu mno akiwa gerezani kama inavyojitokeza katika ubeti wa 101.

Ubeti 101

Mamake kwa hakika
Chakula chema kipika
Asikari humpoka
Chakula wakaila.

Sada ambaye ni mwanamke pia anampelekea Fumo Liyongo chakula kila siku. Kama nguzo ya jamii, wanawake katika utendi huu pia wanatekeleza jukumu muhimu la kushughulikia wanajamii wao hususan wakati Fumo Liyongo anaaga dunia. Wanawake hawa pia wanaonekana wakijishughulisha na mpango wa kuandaa matanga na shughuli zote za kuzikwa kwa Fumo Liyongo alipoaga dunia karibu na kisima. La kushangaza ni kuwa, hatuoni mwanamume yeyote akijihusisha na maswala yoyote kuhusiana na kifo cha Fumo Liyongo. Wanawake hawa pia wanaamua kupashana ujumbe wakati Fumo Liyongo aliaga

dunia. Wanaonekana kujishughulisha na maswala ya kimsingi katika jamii zao ilhali wanaume hawaonekani kamwe. Wakati Fumo Liyongo aliaga dunia, hatuoni wanaume wakitenda lolote kuhusu kifo chake.

Pia katika utendi huu wanawake wanaonekana kuwapasha wahusika wakuu maoni na mwongozo mwafaka ambao kwa kawaida wahusika wakuu wanaufuata. Fumo Liyongo alipoweza kujinasua kutoka gerezani na kurejea nyumbani, mamake anamuonya kuwa asijaribu tena kurejea mwituni akiwa na familia yake kwani alikuwa akihatarisha maisha yake. Hii ni kwa sababu mwanamke huyu alikuwa ameona kuwa Fumo Liyongo alikuwa akikabiliwa na hatari ya kuuawa na maadui wake hususan akiwa mwituni. Mamake alimuonya Liyongo aishi kwao nyumbani ili asihatarishe maisha yake.

Wanawake katika utendi huu wa Fumo Liyongo pia wanaonekana kukereka sana hususan wakati mhusika shujaa anapodhulumiwa. Inadaiwa kuwa Fumo Liyongo alipoaga dunia na ikajulikana kuwa aliuawa na mwanawe, mamake Liyongo alikerwa sana na tendo la kijana huyu. Inadaiwa kuwa alimpigia kelele sana na kuudhika kwa ajili ya tendo la kinyama alilolitenda kijana huyu kwa baba yake.

Ubeti 192	**Ubeti wa 195**
Mamake akaombowa	*Kula siku kumwendeya*
Mashairi akitowa	*Mama wakwe akiliya*
Kwa hasidi kuongowa	*Haunuki saa moja*
Liyongo haya sikiya	*Ni hasira hudhaniya*

Katika utendi huu, wanawake wanaonekana kuwa watiifu na wenye kuaminika. Sada alikuwa ni mhusika mtiifu na mwenye kufuata maagizo aliyopewa. Inadaiwa kuwa mamake Liyongo kila wakati alikuwa akimtuma kumpelekea chakula Fumo Liyongo aliyekuwa gerezani na alitekeleza hayo kwa utiifu na uaminifu wa hali ya juu sana. Fumo Liyongo alipompasha ujumbe ampelekee mamake ili aweze kujikomboa, Sada alitenda hayo bila kununa au kunung'unika. Ni kutokana na utiifu wa Sada ndiposa Fumo Liyongo anaweza kutoweka kutoka gerezani na kujiweka huru. Kwa muhtasari tu, mwanamke katika utendi wa Fumo Liyongo ana jukumu la kipekee sana. Pia, wanawake hawa wanasaidia kuendeleza ploti ya utendi na kukuza sifa za mhusika mkuu, kwa hivyo, wakiondolewa kutoka katika utendi huu, hauwezi kuendelea.

Majukumu ya mwanamke katika Utendi wa Mikidadi na Mayasa

Katika utendi wa Mikidadi na Mayasa, wanawake pia wana jukumu la kipekee na wanatekeleza nafasi muhimu sana katika utendi huu mzima kwani bila wao utendi wenyewe hauwezi kuendelea. Mayasa ambaye ni mhusika wa kike katika utendi huu ana jukumu la kuhakikisha kuwa matendo yote katika utendi huu yanamzingira yeye. Inadaiwa kuwa watu wenye mali nyingi kupita kiasi na umaarufu wa kutajika walitoka maeneo ya mbali ili waje wamuoe Mayasa kama inavyodhihirika katika ubeti wa 27 na 29.

Ubeti wa 27	**Ubeti wa 29**
Walikuja waposi	*Sote tujile kuposa*
Kumuonakwe Mayasi	*Binti yako Mayasa*
Yumo juu ya farasi	*Upendaye mpe sasa*
Jabiri wakamwendea	*Utakae mridhia*

Kwa ajili ya ujasiri wake, Mayasa anawaua wanaume wengi mno na umaarufu wake kuenea kote kote. Mikidadi anadhihirisha sifa zake za kipekee zikiwemo za kinyama akiwa jangwani ili aweze kuyakidhi mahitaji ya Mayasa, hii ni kwa sababu alikuwa akimpenda na

kumdhamini sana. Kuwepo kwa Mayasa katika utendi kunaathiri takribani wahusika wote katika utendi wakiwemo watu wa aila yake kama Jabiri na Turadi. Vilevile, matendo yote katika utendi mzima yanamhusu yeye.

Katika Utendi huu, wanawake wana jukumu la kuwashauri na kuwaonya wana wao. Mikidadi anaponuia kwenda kukabiliana na Mayasa, mamake anamshauri kuwa azimio lake halingefua dafu kwa ajili yeye alikuwa maskini na hakuwa na mali yoyote na pia hakuwa na weledi wa kivita wa kukabiliana na Mayasa. Anamuonya kuwa ingekuwa vigumu kwake kwenda kupigana na Mayasa kwa vile hakuwa na silaha zozote za kivita na alitoka katika jamii iliyokuwa imezama kwenye ufukara kama inavyodokezwa katika beti za 73 na 74.

Ubeti 73	**Ubeti wa 74**
Mamaye akamrudi	*Mali waliotukuwa*
Usiseme Mikidadi	*Yote yamekataliwa*
Tazama wale junudi	*Na wenyewe kuuawa*
Na mali walutukuwa	*Nawe umejionea*

Linalodhihirika pia katika utendi huu ni kuwa mwanamke ameachwa nyumbani na kushughulikia maswala ya kuchunga nyumba na kuwashughulika wanajamii kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Inaaminika kuwa Tamima (mamake Mikidadi) alikuwa akikaa tu nyumbani na kushughulikia maswala ya kinyumbani tu.

Wanawake katika utendi huu wanaonekana kuwa na mapenzi kwa wahusika wa aila yao wakiwemo wahusika wakuu. Inadaiwa kuwa Mikidadi alipokawia kurudi nyumbani baada ya kujitosa jangwani kutafuta mahari ya kulimpia Mayasa, Tamima anaamua kuchukua jukumu la kuripoti kwa aila yake kupotea kwa Mikidadi na kutafuta msaada kwa marafiki wake ili wamsaidie kumtafuta. Anaonekana kuchukua jukumu kubwa la kuungana na wanawake wengine kama vile Hamza kujaribu kutafuta pale alipokuwa mwanawe Mikidadi. Jambo hili linaloonyesha kuwa wanawajali watoto na vizazi vyao. Wanaume hawaonekani kuyajali maisha ya Mikidadi akiwa nyikani ila wanatenda kinyume. Kwa mfano, Malik anataka kumpokonya mpenzi wake alipokawia kurudi baada ya kula njama na Jabiri.

Wake wanachukuliwa kama nguzo kuu katika familia zao kwani wanahakikisha kuwa zinasimama thabiti na kizazi chao kinaendelea. Wanaume wengi waliokuja kwa Mayasa walikuwa wakijaribu kumuoa ili aweze kuendeleza vizazi vyao. Mikidadi anachukua wakati mwingi na kutumia nguvu nyingi ili aweze kumpata Mayasa kwa sababu ingekuwa ni vigumu kuishi peke yake. Baada ya Mikidadi kurejea akiwa na mali nyingi na kumuoa Mayasa, inadokezwa kuwa wawili hawa waliishi kwa raha mustarehe. Hili ni wazi kuwa Mikidadi alipata utulivu baada ya kumpata Mayasa. Pia, inadhihirika kuwa wanawake wanaleta furaha kwa familia zao kama inavyojitokeza baada ya Mikidadi kumwoa Mayasa.

Licha ya Mayasa kuwa mhusika mkuu katika utendi huu, anapewa nafasi finyu tukimlinganisha na Mikidadi. Mayasa kama mhusika mkuu anaonekana kumsababishia Mikidadi shida nyingi kwani takribani matendo yote anayoyatenda, ni kutokana na ari ya kutaka kumuoa Mayasa. Mayasa anakashifiwa sana hasa anapoamua kupigana vita ili ampate mume, lakini hukumu ya Mikidadi si sawa na ya Mayasa. Kwa mijibu wa utendi huu, ni wazi kuwa hitaji la Mayasa la kutaka kupigana na wanaume ni la kijinga na halina umuhimu wowote katika jamii. Licha ya Mikidadi kutekeleza uhalifu wa hali ya juu sana akiwa jangwani, hatumuoni akikashifiwa japo hili ni tendo linalowadhulumu wanajamii wengi wasiokuwa na hatia. Anaonekana tu akisifiwa na kila mmoja na kuchukuliwa kama shujaa.

Katika utendi huu, wanawake wana jukumu la kipekee la kuwakuza wahusika wakuu wanaokisiwa kuwa mashujaa. Inadaiwa kuwa sifa za kivita alizokuwa akizidhihirisha Mikidadi ni kwa ajili ya Mayasa. Mikidadi anatekeleza uhalifu na kuibua sifa za kipekee akiwa jangwani mradi tu aweze kumuoa Mayasa. Weledi wa kivita wa Mikidadi unajitokeza

wakati alipokabiliana na Mayasa katika vita vikali vilivyowashangaza watu wote waliokuwa pale. Pia, umahiri wa Mikidadi wa kukabiliana na makundi makubwa ya kijeshi yanatokana na ari yake ya kutaka kumuoa Mayasa. Vita hivi vikali kati ya Mikidadi na Mayasa vinajitokeza katika ubeti wa 97 na 98.

Ubeti 97	**Ubeti 98**
Wakaingiana kwa kweli	*Na vile wakipigana*
Kwa dhoruba panga kali	*Mato hayajaonana*
Kondo kuu ikatuli	*Ampenda kumuona*
Ikapata muda saa	*Suraze aitambue*

Wanawake wanasawiriwa kama kichocheo cha wahusika wakuu. Katika utendi huu Mikidadi anasafiri safari ndefu kutafuta mali ya kulipa posa iliyohitajika ili aweze kumpata Mayasa. Takribani matendo yote yaliyo katika utendi huu yanachochewa na kuwepo kwa Mayasa ambaye ni mwanamke. Mgororo katika utendi huu unasababishwa na Mayasa.

Katika utendi huu, wanawake wana jukumu la kuolewa na kuwazaa watoto wakiwemo wahusika mashujaa. Mikidadi ambaye ni shujaa anapigana vita vikali mno na Mayasa ili aweze kumuoa. Kwa mujibu wa utendi huu pia, inadaiwa kuwa wanaume walitoka nchi za mbali ili kujaribu bahati yao ya kumuoa Mayasa. Ndoa ina umuhimu wake katika jamii hii kwani inadokezwa kuwa licha ya babake Mikidadi kuwa na mali nyingi na tajiri wa kutambulika, mali yake yote ilitapakaa kila mahali kwa sababu hakuwa na mke na alikuwa na mtindo wa kusafiri kila mahali huku akiiacha bila mlinzi. Inaoneka kuwa wanawake ni wahusika walio na uwezo wa kutunza mali ya jamii kuliko wazee kwa mujibu wa jamii inayosawiriwa katika utendi huu. Suala hili la babake Mikidadi kutokuwa na ndoa thabiti linasababisha Mikidadi kuwa maskini hohehahe.

Hitimisho

Kwa mujibu wa madhumuni ya makala hii, imebainika waziwazi kuwa wanawake wanatekeleza jukumu la kipekee katika tendi ijapokuwa wao wanaangaliwa na kusawiriwa kwa mtazamo hasi. Wanawake katika tendi hizi mbili wana majukumu ya kipekee na wanatenda matendo ya kipekee kwa shujaa na katika tendi zenyewe kwa ujumla. Licha ya majukumu haya muhimu, wao hawadhaminiwa ila wanaponzwa na wanaume katika jamii. Kwa mfano, katika utendi wa Fumo Liyongo, wanawake ndio wanamkomboa Fumo Liyongo kutoka gerezani kwa kumwekea tupa kwenye mkate. Mamake Liyongo anaonekana kutekeleza wajibu wa kipekee wa kumlea Fumo Liyongo, kumpikia chakula na kupanga mazishi yake anapoaga dunia. Licha ya yeye kutenda haya, hadhaminiwa sana katika jamii hii kama ilivyo kwa jagina Fumo Liyongo. Katika utendi wa Mikidadi na Mayasa, Mayasa ni mhusika mkuu kama alivyo Mikidadi lakini umaarufu wake hauenei kama ilivyo kwa Mikidadi. Mayasa anaonekana tu kama mhusika msaidizi na anayemsababishia shujaa na jamii kwa ujumla majonzi.

Kwa ufupi, utafiti huu umehitimilisha kwa kubaini kuwa wahusika wanawake katika tendi teule za Kiswahili wana jukumu na nafasi muhimu sana katika utendi hususan kwa mhusika mkuu lakini wanapewa nafasi hasi (nani anawapa nafasi hasi?) mno ikilinganishwa wenzao wa kiume.

Marejeleo

Allen, J.W.T (mh) (1971) *Tendi.* Bungay: Richard Clay Ltd.

Casco, D. N, (2007) *On epics and its origin.* Australia: Edamund Burke.

Campbel, J. (1949) *The hero with a thousand faces:* Princeton, New Jersey: Princeton University Press.

Carlyle, T. (2001) *On heroes, hero-worships and the heroic in history.* The Pennsylvania State University: A penn State Electronics Classics Series Publication.

Gu'nsberg, M. (1987) *The portrayal of women in the Italian renaissance epics.* Italy: The Italianist Publishing House.

Kruger, G. (1998) The illusion of superiority among humans. *Journal of Personality and Social Pychology, 77* (6): 1121-1134.

Mulila, J. (2009) *Usawiri chanya wa wahusika wanawake*. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi, Kenya.

Lynns K.M. (2009) *Critical analysis of Campbell heroic archetypal*. New Jersey: Prentice Hall

Mulokozi, M. M. (1996) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili;* OSW 105. Dar es Saalam; Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.

Rank, P.W. (1999) *Discourses on ancient heroic works*. Harlow: Longman.

Senkoro, F. E. M. K. (1987) *Fasihi na jamii*: Dare es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1987) *Ushairi, Nadharia na Uhakiki*. Dare es Salaam: Press and Publicity Centre.

Wamitila, K.W. (2003) *Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

Mohamed, F. A. (2016) *Kuchunguza mila na desturi za mwanamke wa visiwani pamoja na fani katika tenzi za howani na mana Kukuwa.* M.A. Thesis, Chuo Kikuu cha Huria Cha Tanzania.

Ndung'u, J. N. (2016) *Tathmini ya ushujaa katika tendi teule za Kiswahili: Mfano, utendi wa Fumo Liyongo, Utendi wa mikidadi na mayasa na utendi wa swifa ya nguvu mali*. M.A. Thesis, Chuo Kikuu Cha Laikipia, Kenya.